# NAFASI YA MAAFISA RASLIMALI WATU NA UTEKELEZAJI WA AWAMU YA NNE YA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI (NACSAP IV) 2023-2030

JULAI 23, 2025

POKELA, FABIAN S.
(0655255227)



# Yatakayojadili wa

1. Utangulizi

2. Mantiki ya Dhana ya Maadili, Uadilifu na Rushwa (Corruption)

3. Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne na Historia yake

4. Hitimisho



# 1.0 Utangulizi


-**Lengo la Serikali** ni kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa Umma kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatamka wazi kuwa "**Jukumu la Serikali ni Ustawi wa Wananchi wake**"

-**Dhana ya Serikali** inahusisha Sekta muhimu ya Watumishi wa Umma na msingi wake ni mkataba wa Serikali na wananchi kwa lengo la kuhakikishiwa Ulinzi wa Uhai wao, Mali zao (**Za Umma)** na Maendeleo yao.

-**Dhamana ya Maafisa raslimali watu** ni Kusimamia Utendaji na tabia zinazoambatana na utendaji wa watumishi ambayo ndio dhana kuu ya **uadilifu**



# Uhusiano wa Maafisa Raslimali watu, Serikali na Wananchi





# 2.0 Mantiki ya Dhana ya Maadili, Uadilifu na Rushwa

***Maadili*** = Sheria, kanuni, Taratibu, Mila, Desturi zinazoongoza namna ya Utendaji wa Watu

***Uadilifu*** = Hali ya ndani ya mtu na sifa ya kuzingatia Maadili katika mazingira yote (**Doing the right thing)**

***Rushwa (Corruption)*** = Hali ya ndani ya Mtu kukosa uadilifu na kutoa matunda mengi maovu

# Dhana ya Uadilifu na Rushwa





# Nini Nafasi ya Maafisa Raslimali watu katika kukuza Uadilifu na Juhudi dhidi ya Rushwa katika Utendaji Serikalini?

- Hatua za Serikali katika kuhakikisha utendaji adilifu na juhudi dhidi ya Rushwa zimesababisha kuwepo kwa Mkakati wa Kitaifa ili Kukuza uadilifu na kuwa na Afua dhidi ya Rushwa.
- Mkakati huu wa Kitaifa unapaswa kuchukuliwa kama kitendea kazi (Support tool) kwa Wasimamizi wa Raslimali watu wanaotambua vyema dhamana na nafasi yao Serikalini)

# 3.0 Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV) na Historia yake

- Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ni mwendelezo wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ambao umetekelezwa kwa awamu 3 kuanzia Mwaka 2001 mpaka Juni, 2022;




Awamu ya Kwanza ya Mkakati **(2001-2005**) ililenga kujenga Mifumo ya Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi katika utoaji wa huduma kwa Umma



- Awamu ya Pili ya Mkakati **(2006 -2011)** ililenga kuimarisha mifumo iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza ya Mkakati na kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma Serikalini *(Government business re-engeneering)*



Hii ndio sababu ya Awamu ya Pili kutekelezwa sambamba na Programu za Maboresho kama vile PSRP, LSRP, LGRP, FSRP, PFMRP, BEST-Roadmap  na ASDP.



Awamu ya Tatu ya Mkakati (**2017-2022**) ililenga kupunguza rushwa nchini kwa:

a) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji huduma katika sekta ya umma na binafsi;
b) Kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mkakati wa mapambano dhidi ya rushwa;
c) Kuzijengea uwezo Taasisi Simamizi za mapambano dhidi ya rushwa;
d) Kuwa na Uongozi Madhubuti wa kisiasa unaoshiriki kwa dhati katika mapambano dhidi ya rushwa.



**Lengo Kuu** ni Kuwa na Jamii Iliyostawi na yenye Mifumo Madhubuti ya Kukuza Uadilifu na Isiyovumilia Rushwa.



## Malengo Mahususi ya Mkakati

(1) Kuwezesha Jamii kushiriki kikamilifu katika juhudi za kukabiliana na rushwa na kuimarisha uadilifu;

**(2)** Kuimarika kwa uwajibikaji na uwazi katika Taasisi za Umma na Taasisi Zisizo za Kiserikali**;**



(3) Kuimarika kwa uwezo wa Taasisi za Utawala Bora ili ziweze kukuza uadilifu na kukabiliana na vitendo vya rushwa;

(4) Kukuza matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma wa Taasisi za Umma na Taasisi Zisizo za Kiserikali;



**(5)** Kushirikishwa kwa Taasisi Zisizo za Kiserikali katika kukuza uadilifu na kukabiliana na rushwa nchini.

**(6)** Kuimarika kwa uadilifu wa usimamizi wa mchakato wa uchaguzi wa kisiasa usio na rushwa.



# MPANGILIO WA KITAASISI

1. Ngazi ya Taifa

2. Ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za
   Serikali za Mitaa

3. Taasisi zisizo za Kiserikali



## (i) Ngazi ya Taifa

### (a) Kamati ya Taifa ya Uendeshaji

Kamati hii itasimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne na Mpango wa Utekelezaji.



**(b) Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Kitaalamu**

Wajumbe wanateuliwa kutoka katika Taasisi simamizi za Utawala bora



## Idara ya Uratibu wa Utawala Bora na Maboresho

Idara hii itakuwa ni kiungo kati ya Katibu Mkuu Kiongozi, Ofisi ya Rais Ikulu na wadau wa utekelezaji wa Mkakati;





## Utekelezaji wa Mkakati katika Ngazi ya Taasisi

Kutakuwa na Kamati mbili za uratibu wa utekelezaji wa Mkakati katika ngazi ya Taasisi za Umma na Taasisi Zisizo za Kiserikali ambazo ni

**(a)** Kamati Maalum ya Menejimenti

**(b)** Kamati ya Uadilifu.

# Kamati Maalum ya Menejimenti

**-**Mtendaji Mkuu ndiye Msimamizi Mkuu

- Katibu ni Mkuu wa Idara HR

-Mwenyekiti wa Kamati ni Mwalikwa

- Mtendaji Mkuu awasilishe Taarifa ya Kila robo kwa Katibu Mkuu Kiongozi



-Wajumbe wa kamati watakua wenye sifa ya Afisa Mwandamizi mwenye haiba ya uadilifu;

-Wajumbe watatumikia nafasi zao kwa kipindi chote cha Utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mkakati.

-Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa Taasisi atakuwa huru kubadilisha wajumbe wa Kamati ya Uadilifu atakapokuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo;

***-Idara inayohusika na Utawala na Rasilimaliwatu itakua ndio Sekretarieti ya Kamati ya Uadilifu***.



# Kamati ya Uadilifu ya Taasisi

-Kamati ya Uadilifu ya Taasisi itakuwa na wajumbe watano watakaoteuliwa na Mtendaji Mkuu wa Taasisi akiwemo Mwenyekiti na Katibu;

-Miongoni mwao atakuwepo mjumbe mmoja kutoka nje ya Taasisi ambaye ikiwezekana awe mjumbe wa Kamati ya Uadilifu katika Taasisi anayotoka na atapatikana baada ya maombi ya Taasisi nufaika;

***-Katibu wa Kamati atakuwa ni Afisa Mwandamizi kutoka Idara inayohusika na masuala ya utawala na usimamizi wa rasilimali watu ya Taasisi.***



-Muda wa Utekelezaji wa Mkakati ni miaka saba (**2023-2030)**

-Taasisi za Umma zitawasilisha Taarifa ya Utekelezaji ya robo mwaka na mwaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Taarifa hizi zitachakatwa na mrejesho kutolewa kwa wahusika


-Taarifa ya Utekelezaji ya Taasisi Zisizo za Kiserikali itawasilisha kwa Katibu Mkuu ***Kiongozi kupitia Taasisi Rekebu***.



# 4.0 HITIMISHO

- Ni matarajio ya Serikali kuwa kila mwananchi kwa nafasi yake atashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mkakati huu ili kuiwezesha Serikali kutekeleza ipasavyo jukumu lake la Kikatiba **(Ibara ya 8(1) (b) la kuhakikisha ustawi wa wananchi wake**.

- Maafisa Utumishi wenye dhamana ya kusimamia uadilifu na utendaji wa watumishi wa Umma wanatarajiwa kuwa vinara katika kuhimiza na kusimamia utekelezaji wa Afua za Mkakati kikamilifu ili kuweza kufikiwa kwa malengo tarajiwa ya Mkakati.


CARR TIDE PORT VILA
alamy
24/07/20
Image ID: KB5D9A
www.alamy.com



# ASANTENI

Pokella, Fabian S

fabian.pokela@maadili.go.tz

0784-255227